JUA

GAZETI LA MAENDELEO

Kiongozi: Mutiri-wa-Bashara - Mwaka wa 21 - Toleo la 447

Masikilizano ya Kinshasa

# Waziri mkuu ni Tshisekedi ao nani ?

Mjini mkuu Kinshasa ambako mabingwa wa siasa nchini Zaïre wa pande mbili, hao wa upinzani (USOR) na wenzio wanaomuunga mkono Raïsi wa Jamuhuri Mareshali Mobutu Sese Seko (FPC) haijajulikana bado nani atakaye ongoza inchi akiwa waziri mkuu kiisha masikilizano inayoendeshwa kunako jumba la raïa.

Masikilizano haya iliyoaminika kumalizika kiisha mda wa siku nane sasa yameendelea mpaka kufikilia juma ama wiki tatu na zaïdi. Ingawa wahuzuriaji kunako mkutano huu wamekwisha kusikilizana kama wandugu kunako matatizo fulani za mbele, yasemekana kunako chumba la Raïa ama "Palais du Peuple" kuwa wanasiasa hawaelewani kwa jambo limoja. Ni nani kati ya Birindwa na Tshisekedi atakayetajika waziri mkuu. Wapinzani waitaji na kupiga kelele ya kumuunga mkono ndugu Etienne Tshisekedi wa Mulumba ambae amechaguliwa tangu hapo zamani kidemokrasia na wahuzuriaji kunako mkutano mkuu (Conférence nationale). Na ambaye angojewa na raïa na kuchukiliwa na Raïsi Mobutu pia wafwasi wake.

Mpinzani huyo ajulikana nchini Zaïre kama vile mwenyi siasa kali na ujuzi pia mamlaka yakuweza kumpindua kisiasa mareshali Mobutu kwa kuwa yeye apendwa na raïa inayomuunga mkono, wasemavyo wenzio wanasiasa ya Muungano mtakatifu (USOR) wa upinzani inchini Zaïre.

Lakini hakuna tatizo lolote kuhusu jina la Mobutu na lile la askofu Monsengwo kwa uongozi wa taïfa na wa Muungano wa Washauri (HCR-P) unaoitwa sasa "Mungano wa Washauri na Mabunge wa Taïfa" kiisha masikilizano. Tatizo ni lile lakuamua : isipokua Tshisekedi, itakuwa nani ? Je, Mbona raïa wateswa na njaa, wafanyakazi wa serkali hawapokei mishahara yao imepita hata miezi sita, kumi na zaïdi ? Je, kiti cha Waziri mkuu kimegeuka kibuyu ao chupa ya chumvi ambamo utamu haumalizike na ambao siyo ya kuachia wengine ?

Twawaomba wanasiasa wawaonee raïa huruma na mzozo wa mji mkuu Kinshasa ukome. Wanamemba 760 wa "Mungano wa washauri na wabunge wa Taïfa" wafanye haraka kutoa raïa utumwani mwa njaa na fujo inayoletwa na wanasiasa nchini mwetu.

Imata Raphaël Déwen

# Yamefungulia mitaani Uvira na Fizi

Mwaka huu wa masomo 1993-1994 umefunguliwa kwa masomo ya kipekee (privées). Lakini mengine ya kiserkali na hayo yasimamiwa na makanisa yangali bado na matatizo kutokana na kutolipwa kwa walimu na hata ya wazazi watumishi wa serkali na wengineo. Ni toka hayo twajiuliza kama masomo yatafunguliwa kweli.Hata kama "Institut" Hekima ya wa kimbanguiste pa Uvira na Alfajiri pa Bukavu zimefungua tangu mbele, ni vizuri tujulishe kama masomo yote ya mitaa ya Uvira na Fizi zimefungua milango yao tangu tarehe 4/10/93.

Baada ya uchunguzi tulioufanya imeonekana kuwa kuhusu hali ya nyumba ya watenda masomo mengi vimeharibika vikali. Masomo hayo yamekuwa nyumba ya watenda maovu, wavutaji wa bangi na hata vyoo kwa wapita njia .

Masomo mengine yameundwa kwa nia tu pupa ya feza. Imeonekana pia kuwa masomo hayo, ya msinji, ya segondari na ya kiufundi yaundwa popote ingawa hayatimizi shurti. Huko malipo ni ya mwende mukaone. Je, leo hii walimu huko walazimisha kulipwa mishahara ya zaäre 200.000.000 na zaidi ingawa wazazi watafunga mkaba na huo ? Kumbe kwa siku za leo, wazazi watafunga mkaba na kuukaza pia kuchagua kati ya watoto nani apate kusoma. Bei ya vyombo na vifaa vya masomo ni kali na yapandishwa kwa mwendo wa kunguru wazazi wasijue la kufanya. Watoto wengi wamegeuka wachuuzi wa rejareja, wevi na wengineo watenda maovu. Wakidai kwamba ni feza zitakazosema wakati wa mashindano. Walimu kwa ngambo yao wamekuwa wakosefu na wa "mendiants" wakidoeadoea na kuomba misaada popote kama wamaskini.

Kwa kweli, viongozi wa makanisa, wa masomo, walimu na wazazi wakutana mara nyingi bali ni kugumu kupata jawabu. Viongozi wamoja wasema kuwa wazazi walio na pato ndio watoto wao wataweza kufundishwa. Hiyo yakwenda kinyume na sheria na mahitaji ya umma pia na mapaswa ya serkali. Serkali ambayo yapaswa kuhusika na maelimisho pia maadibisho ya wafanyakazi wa kesho. Walimu kama vile wazazi na wanafunzi wapo, kwa sasa, na afia mbovu. Ijapokuwa wote wapaswa kuwa na afia njema ili kazi zao zifikilie kutoa matunda mazuri.

Kutokana na magumu wanayo wazazi, walimu, kupitia njia ya "syndicat" yao, wamekwisha kusudia kutofundisha mpaka hapo serkali italipa mishahara kwa wote. Na serkali kweli imehaidia kulipa mishahara hiyo mbele ya mwisho wa mwezi wa septemba.

Basi tukingojea jawabu toka viongozi, tumuombe Mungu Mweny'Ezi atusaidie kwa magumu yatuangamiza na yapate kurahisishwa kwa uwezo wake.

André Bisimwa L-B Tserou

# Arkiaskofu Mulindwa ajiuzulu

Kulingana na habari zinazoaminika, Baba Mtakatifu wa Roma, Papa Yoane Paulo wa Pili, atoka kumtaja Askofu Munzihirwa Mwene-Ngabo wa Kasongo kama vile kiongozi kwa mda wa arkidiosezi ya Bukavu akimgombwa hivi Arkiaskofu Mulindwa Mutabesha ambaye atoka kujiuzulu. Mheshimiwa arkiaskofu Mulindwa aliongoza arkidiosezi ya Bukavu tangu mwaka wa 1966 hadi leo hii. Askofu Munzihirwa, kama vile kiongozi mpya (administrateur) wa arkidiosezi ya Bukavu, ataongoza Mkutano wa maaskofu wa jimbo la kidini katoliki la Kivu ikingojewa kutajwa arkiaskofu mpya wa Bukavu .

Askofu Munzihirwa alikuwa hapo zamani padri mkubwa wa parokia kunako katedrali ya kikatoliki ya Bukavu mbele aingie katika shirika la mapadri wa "jésuites" na hata kafikilia kuwa padri mkuu wa mapadri hao katika Afrika ya kati (Burundi, Congo, Rwanda na Zaïre)

Mheshimiwa Askofu Munzihirwa ni mzaliwa wa mkoa wa Mbiza, parokia ya Mbobero katika mtaa wa Kabare na askofu wa Kasongo tangu miaka mitatu sasa .

Baada ya miaka 27 kama vile kiongozi wa arkidiosezi ya Bukavu, arkiaskofu Mulindwa aweza sasa kupumzika katika heri. Kama vile mwenzie askofu Pirigisha, hapo zamani askofu waKasongo, ataweza kusaidia umma la kikristiani kutokana na maarifu na ujuzi wake katika mambo ya kidini na kijamii.

Arkiaskofu Mulindwa anaacha kazi kufuatana na uzee wake pia afia yake mbovu, siyo sababu ya tabia yake fulani kadiri watu watangaza.

André Bisimwa L-B. Tserou

## UHARIRI

# Maisha mazuri

Kitu kizuri gani twaweza kutumainia toka mkutano wa masimulizi na mabishano kati ya wanasiasa ? Kweli hakuna chochote! Kwani, wakati wanasiasa wawili, watatu na kazalika wakutana ni kwa nia tu ya kutafuta ginsi gani watagawa madaraka ya uongozi wa nchi na kukinga faida zao wenyewe .

Lakini kama Mwana-Zaïre asahau shuruli zake za kila siku na kungojea matukio ya masimulizi na mabishano yafanyika kunako Jumba la Raïa ama "Palais du peuple" ni kwa sababu ameona kuwa magonvi ya wanasiasa yaendelea kuleta vurugo na uwasiwasi nchini.

Hali ya maisha nchini yatokana na matukio ya magomvi hayo ya wanasiasa yasiyo na mwisho. Ukweli ulioko ni kuona kuwa Mwana-Zaïre atafuta kwanza na mbele ya yote kuwa na maisha mazuri. Apate kula mara mbili ao mara tatu kwa siku, kuwa na mshahara wa kutosha, shurti nzuri za kazi, kwa kifupi kuwa na namna ya kuishi ginsi ifaavyo na ambayo hapate kutokana na ukosefu na magumu ya maisha ambayo Mungu Muumbaji kaitolea mali mengi ajabu, haikubaliwe Mwana Zaïre hasifaidie mali hayo mengi.

Ni hiyo angojea toka masimulizi na mabishano yafanyika na wanasiasa kunako Jumba la Raïa : Maisha Mazuri hapo makesho .

André Bisimwa L-B. Tserou

# Je, umesikia ... ?

**KUWA,** viongozi wa chumba kihusikacho na mambo ya arzi na wale wa ujenzi bora wa jimbo ya Kivu ya Kusini wapaswa kujiuliza kwa nini kawauzishia wafanyabiashara wakuu wa hapa Bukavu na wengineo eneo la kimakao ya raïs wa jamhuri lipatikanalo mtaani Ibanda, karibu na makao ya liwali wa jimbo ? Bwana liwali wa jimbo asisitiza kuwa bwana Yassa Ekofo, aliyekuwa kiongozi wa chumba cha arzi ndiye msinji wa jambo lile. Hata hivyo, mkataba uliotiwa saihi na chumba cha liwali wapiga marufuku kitendo kile. Twazani kuwa liwali Kyembwa atafanya yote kwa ajili ya kukomesha sheria za ujenzi sio tu wa mahali hapo bali pia wa mahali mengine yasiyostahili kwa kuepuka misiba.

**KWAMBA,** kunako chuo cha Alfajiri, mambo hayaendeki wakati masomo yatarajiwa kufunguliwa ? Mikutano kafanyika kati ya wakuu wa masomo, wazazi na walimu haikuweza kufanyika kufaulu. Hata hivyo kufunguliwa kwa masomo kwaleta uwasiwasi. Huko mwalimu moja kafukuzwa kwa vile kauliza malipo ya mwalimu ambayo sehemu moja ya pesa yatoka ugenini. Mahakama yashurulika na jambo lile sasa.

**ETI,** ni vingi vyama vya kisiasa na mahali pa kuendesha kazi zao? Hata vile vyazaniwa vikuu na vya kujiheshimu. Yasemekana kuwa vingi kati yao vyapanga ndani ya nyumba ya viongozi wao, hoteli, vilabu na penginepo kwa wanamemba. Kama tungelisema kuwa vyama hivyo vyapangishwa vizuri sana. Watu hujiuliza kama si hali ya kukimbia kutendewa maovu na watu wakati huu ambao halmi ya siasa yapamba moto ? Ukweli upo wapi wakati twajua kama chama cha siasa chaweza kuvunja uhusiano wa viongozi wake !

**KAMA,** wachuuzi na wasafiri toka Bukavu kuenda Uvira kupitia barabara ya Ngomo wamefurahi kuona kilalo kilicho katika hapo majuzi kutengenezwa na wakaaji. Kwa kuwa kunako forodha (Douane) ya Kamanyola na Ruzizi II watumishi wa shirika la OFIDA, Gasutamo, SNIP na OZAC walikuwa wamekwisha furahi na kulipisha gari na wasafiri pesa za kimagendo na kuwafyonza sana.